

CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO



NDAKI YA MISITU WANYAMAPORI  
NA UTALII

TRICHILIA EMETICA -NATAL  
MAHOGANY

(MGOLIMAZI, MDODOMA)

Family: Meliaceae



Kimetolewa na  
Ndaki ya Misitu Wanyamapori na Utalii,  
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,  
S. L. P 3009,  
Chuo Kikuu,  
MOROGORO TANZANIA  
Tel. Gen. Line 255 023 2603511/4 Ext. 4601  
E-mail: forestry@suanet.ac.tz

Ni mti usiopukutisha majani, hivyo huwa kijani muda wote. Maua yake huwa na harufu nzuri, hivyo ukipandwa bustanini hukaribisha nyuki na ndege wazuri.



Matunda ya *Trichilia emetica*

#### Maelezo

1. Mti unaokuwa kijani muda wote.
2. Ni mti usiorefuka sana, hufikia urefu wa mita 20
3. Huwa na miti ya kiume na kike
4. Maua yake huvutia ndege wa aina mbali mbali
5. Matunda yake huliwa na wanyama kama nyani na swala



#### Matumizi

##### Dawa:

1. Unga unaotokana na gamba la *Trichilia emetica* katika maeneo mengine hutumika kama dawa ya tumbo. Gamba pia huweza kutoa rangi ya pinki (pinkish dye).
2. Mizizi inaweza kutumika kama dawa ya homa.
3. Majani au matunda hutumika kama dawa ya ugonjwa wa ngozi (eczema).
4. Mafuta kutoka katika mbegu huweza kutumika kulainisha ngozi (moisturise) na pia kutengeneza sabuni.
5. Mafuta pia hutumika kutibu 'rheumatism' na kufunga katika vidonda.

\*\* Ganda la mbegu zake ni sumu.



Mafuta ya *Trichilia Emetica*

#### Matumizi ya mti wenyewe

1. Kutengenezea vinyago vya kiutamaduni kwa jamii kusini mwa Afrika.
2. Kutengenezea vifaa vya muziki, fanicha na mitumbwi.
3. Katika maeneo mengine pia hutengenezea vifaa vya kiutamaduni kama bakuli, masinia na vijiko.
4. Mti wa kivuli kwa wanadamu na wanyama – Huoteshwa katika bustani.
5. Hupandwa kuzuia upepo mkali (Wind break).

#### Ukuzaji

*Trichilia emetica* ni mti unaokua haraka na unaweza kuoteshwa kiipindi kirefu cha mwaka;

1. Unaweza kuvumilia hali mbalimbali za hewa kama baridi sana, ukame na mvua nyingi.
2. Huoteshwa kutumia mbegu (fresh seeds). Wakati mwingine uoteshaji huweza kuwa mgumu.
3. *Trichilia emetica* haupendi kivuli kilichozidi bali cha wastani na sehemu wazi zenye jua



Mti wa *Trichilia Emetica*